**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (OWM- TAMISEMI)**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO MWAKA………………….**
**SHULE YA SEKONDARI NANGA, S.L.P. 108, IGUNGA**

***"Moto" wa Shule:*** ***Elimu ni Kazi***


***Mawasiliano;***
**"E-Mail" ya shule:** ***hmnangasec@yahoo.com Mkuu wa Shule:stephenmzimya@gmail.com***
**Mkuu wa Shule: 0755 428 626 / 0735 428 626 / 0782 728 427**
**Makamu Mkuu wa Shule 06213221263**
**Matron: 0762 968 347/0623 920 337**
**Patron: 0624 318 516**
**Msajili wa wanafunzi 0652454013/0615980659**

**OFISI YA WAZIRI MKUU- TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (OWM-TAMISEMI) HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA**

**SHULE YA SEKONDARI NANGA,**
**S.L.P 108,**
**IGUNGA.**
**TAREHE ...............................**

**KUMB.Na . HWIG/NSS/F.V-2025/26/10**
**Jina la Mwanafunzi;**

**………………………………………………………………………………………**
**S.L.P. …………………………………………………**
**…………………………………………………**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO MWAKA………………...**

1. Ninayo furaha kukuarifu kwamba Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (**OWM-TAMISEMI**) imekuchagua kujiunga na kidato cha **TANO (Tahasusi ya..........)** katika Shule ya Sekondari Nanga, iliyoko Wilayani Igunga, Mkoa wa Tabora. **Hongera sana.**

**Mahali Shule ilipo:**
Shule ipo Km 52 kutoka Nzega na Km 32 kutoka Igunga kwenye barabara kuu ya lami ya Mwanza - Dar-es-Salaam. Shule ipo Mita 300 tu kutoka barabara kuu ya lami kilipo kibao cha Shule (**Sign Block**). Shule hii ni ya mchanganyiko wavulana na wasichana. Wavulana wote wa Kidato cha I-IV wanasoma Kutwa.Wasichana na Wavulana wa kidato cha V&VI;Wote wanakaa Bweni.

**Usafiri;**
Usafiri wa kufika Nanga ni wa Mabasi yapitayo kila siku kwenda na kutoka Dar es Salaam-Mwanza. Endapo utashukia Igunga Mjini utapanda magari madogo yaendayo Nzega na utashukia Nanga kilipo kibao cha Shule na kutoka Nzega utapanda magari madogo yaendayo Igunga na utashukia Nanga kilipo kibao cha Shule.
Unatakiwa kufika Shuleni siku moja kabla ya Kufungua Shule**. (Epuka kufika Usiku)**.
Unapofika Shuleni hakikisha kuwa unaleta mahitaji yote yaliyoelekezwa katika barua hii.
Mwisho wa kuripoti ni tarehe ........................................
Aidha wanafunzi wote watakaokuwa wanalipiwa michango na mamlaka au mashirika mbalimbali kama vile *Serikali Kuu,Halmashauri za vijiji,Wilaya,Miji,manispaa,Jiji au Wafadhili* wengineo watapaswa kuja na barua za wafadhili wao ili kuweka kumbukumbu sawa za mpango wa malipo ili **wasikwamishe uendeshaji wa Shule na huduma kwa wanafunzi husika.**

## 2.0: MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA: -

### 2.1: SARE YA SHULE

**A) WASICHANA:**

i. Sketi 2 nyeusi "***kitambaa kizito***"zenye malinda 16 (Kumi na sita) ya kupanga,ziwe zinafunika
ii. **KIFUNDO** cha miguu karibu na nyanyo zisizobana mwili, na mkanda wake usiozidi inch (2) (beriti).
iii. Mashati mawili ya mikono Mirefu meupe yasiyo na maua,yasibane mwili. Shati ichomekewe
iv. ndani ya sketi wakati wote.
v. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba visivyofanana na buti vyenye kutumia kiwi na sio petroli vyenye visigino vifupi. (Viatu vya ghorofa haviruhusiwi kabisa)
vi. Soksi nyeupe jozi mbili ndefu
vii. Tai ndefu ya rangi nyeusi.
viii. Sweta la mikono mirefu 1 **Rangi ya Bluu**. (Sweta Lisiwe na maua ya aina yoyote).
ix. Wasichana wa Kiislamu wanaopenda kuvaa Hijab wakati wa masomo wanaruhusiwa.
x. Kushona sketi ndefu rangi ya sare ya Shule (kitambaa kizito) na Blauzi nyeupe mikono mirefu (nusu kanzu) na blauzi rangi ya bluu mikono mirefu (nusu kanzu)

**B) WAVULANA**

i. Suruali mbili (2) nyeusi kulingana na urefu wako na iwe pana ya kutosha.Upana wa chini usipungue 20cm, ukunjwe kwa pindo la nje (*TurnUp)*. Isiwe ya kubana na mifuko yake iwe ya pembeni, siyo ya mbele aina ya (*Pisto)* ni marufuku uvaaji wa suruali chini ya makalio.
ii. Mashati mawili(2) meupe ya mikono Mirefu, yasiyo na maua,yasibane mwili. Shati ichomekewe ndani ya suruali wakati wote.
iii. Mikanda iwe ya heshima ya rangi nyeusi ya ngozi isiyokuwa na picha wala urembo wowote.
iv. Tai ndefu rangi nyeusi .
v. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba visivyofanana na buti vyenye kutumia kiwi na sio petrol, viwe na visigino vifupi, viatu vya ghorofa haviruhusiwi.
vi. Sweta la mikono mirefu 1 **Rangi ya Bluu**. (Sweta Lisiwe na maua ya aina yoyote).
vii. Soksi nyeupe jozi mbili .

### 2.2: NGUO/SARE ZA MICHEZO NA KAZI (Shamba Dress)

**(a) Wasichana**

i. Sketi mbili ya **light blue** na nyingine nyekundu. Ashone kwa kufuata maelekezo kama
ii. yale ya sketi nyeusi (kitambaa kizito malinda (16) urefu unaofunika kifundo cha mguu za kuvaa wakati wa michezo, kazi za nje na wakati wa masomo ya jioni
iii. Raba za kuvaa wakati wa michezo, kazi na wakati wa masomo jioni; Rangi yoyote
iv. Track suit rangi **Bluu.**
v. Bukta 1 rangi ya **Bluu**.

**(b) Wavulana**

i. Suruali mbili za rangi ya **Bluu Bahari** (Light blue) zishonwe kwa kufuata maelekezo ya
ii. suruali nyeusi. Hatua kali zitachukuliwa kwa ambaye hatazingatia mashariti ya ushonaji
iii. Raba za kuvaa wakati wa michezo, kazi na wakati wa masomo jioni; Rangi yoyote
iv. Bukta 1 ya rangi ya **bluu .**
v. Track suit rangi ya **bluu .**

**3.0: MAHITAJI YA BWENI. (WAVULANA NA WASICHANA)**
Vifaa vifuatavyo ni vya Lazima kwa Mwanafunni kuja navyo Shuleni.

i. Godoro Moja futi (2.5-Upana), Chandarua pamoja na Mto.Rangi za foronya za mito zifanane na rangi za mashuka.
ii. Vyombo vya chakula; Sahani yenye Vyumba-vyumba ya Chuma (**Aluminum Tray**), Kikombe na Kijiko tu!.
iii. Shuka mbili {**Blue Bahari***(Light Blue na* Rangi ya *Pink* )}.
iv. Ndoo moja (01) ya Plastiki. (Lita 10).
v. Ndoo kubwa moja (1) za plastiki (za ujazo wa lita 20) (Wasichana na Wavulana) kuwa na sabuni za kutosha kwa usafi binafsi Fagio la nje lenye mpini wote, fyekeo kwa wavulana, mopper kwa wote na fagio la ndani (soft bloom) kwa wasichana.
vi. Bunda la karatasi A4 **(double A tu na sio aina nyingine )** moja kila muhula (2 kwa mwaka)
vii. Jalada (folder file) kwa ajili ya kutunza kumbukumbu za mwanafunzi
viii. Tochi kwa tahadhari ya kukatika umeme (taa ya kuchaji kwa jua inafaa zaidi)

**NB*:Mwanafunzi haruhusiwi kuja na Mizigo Mingi zaidi ya begi 1 dogo la Mgongoni (begi la shule) na Sanduku 1 la Chuma (Tranka). Hakuna nafasi ya Kuhifadhi Mizingo Mingi bwenini***

**4: MICHANGO MBALIMBALI**
**MAELEKEZO YA MICHANGO MBALIMBALI**
Michango inatakiwa kulipwa kupitia **Benki ya NMB Namba ya Akaunti 50901100022**
**Jina la Akaunti – NANGA SECONDARY SCHOOL RECURRENT. A/C**
Mwanafunzi lazima *alete fomu aliyotumia kuweka fedha Benki**(Bank Pay in Slip)*** inayoonesha umelipa mchango/ ada hiyo, jina la mwanafunzi, kidato vinapaswa kuonekana katika hiyo *Bank Pay in Slip*.
**NB:***(Lipa Tawi lolote la NMB au wakala wa NMB aliyeko karibu na wewe).*

**JEDWALI LA UFAFANUZI WA ULIPAJI WA MICHANGO**

| NA | AINA YA MCHANGO/ KIFAA | KIASI TSHS |
|---|---|---|
| **1** | Uendeshaaji wa shule | Tshs 65,000/= |
| **2** | Tahadhari (*Haitarudishwa)* | Tshs 5,000/= |
| **3** | Kitambulisho na Picha za Mwanafunzi | Tshs 5,000/= |
| **4** | Nembo | Tshs 5,000/= |
| | **JUMLA** | **Tshs. 80,000/=** |

**NB:**Mwanafunzi anatakiwa aje na Vifaa vya kutosheleza vya Kujifunzia darasani; yaani **Daftari-**kubwa *(Counter Books*) za Kutosha masomo kulingana na idadi ya masomo utakayosoma **Vitabu-**mzazi mwenye uwezo anashauriwa kumnunulia mwanae **vitabu** kulingana na Tahasusi anayosoma mwanafunzi(walau kitabu kimoja kwa kila somo kulingana na uwezo wa mzazi) **Vifaa** vingine kama Kikokotoo(**Scientific calculator**) kwa watakaosoma masomo ya Sayansi pamoja na **Dissecting Kit** kwa wanafunzi watakaosoma somo la *"Biology"* na bunda la karatasi ya mistari kwa matumizi yake kwa ajili ya mitihani ya kila wiki na mwezi. Wanafunzi wa kiingereza wanapaswa kuwa na **Advanced Learners Dictionary**. Kufuatia maboresho ya mtaala unaoanza mwaka………………… mzazi anaweza kumpatia laptop (kompyuta mpakato) kwa ajili ya kujifunza na kutafuta vitabu.

**NB: Ni muhimu Kila mzazi kumkatia mwanafunzi bima ya matibabu bima ya afya ni Tshs. 50,400/= kwani suala la matibabu ni jukumu la mzazi au mlezi. Wenye kadi za bima waje nazo.**

Ili kuepusha usumbufu wa kubeba vifaa vingi wakati unasafiri kuja shule, tunashauri uje ununue baadhi ya vifaa hasa vya "Stationaries" Mfano; **Madaftari** Makubwa (Counter Books); **Scientific calculator** pamoja na mahitaji mengine kama **Masweta,Fagio la ndani, Fagio la Nje, Rimu, folder file** pamoja na **Mahitaji mengine madogo madogo** kwa Mwanafunzi; -vinapatikana kwenye duka la shule kwa bei nafuu. Msimamizi wa duka namba yake ni ***0623920337***

## 4.0: SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.

### 4.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kumiliki wala kutumia simu shuleni kwa akikutwa nayo atafukuzwa shule.**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**5.0: MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Wanafunzi wote (wasichana na wavulana)wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi au vifaa vya simu katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**6.0: MAMBO MENGINE MUHIMU:**


Mwanafunzi anaporipoti, anatakiwa aje na ***Mzazi/Mlezi*** pamoja na fomu hizi za maagizo ya kujiunga na Shule zikiwa zimejazwa.Vinginevyo hatapokelewa.Fomu zote zijazwe kama ilivyoelekezwa;na atatakiwa kuzikabidhi kwa Makamu Mkuu wa Shule mara atakapo ripoti Shuleni.

a. **Medical Examination Form**: Fomu hii itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali baada ya kukupima kwa uthibitisho halisi wa afya yako .
b. **Fomu ya Maelekezo binafsi:**Fomu hii itahusu historia ya Mwanafunzi/ Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai .
c. **Fomu ya Mzazi** kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, na maelekezo mengine yatakayotolewa na Shule.
d. **Picha Nne (04)** za wazazi/Walezi au ndugu wa Karibu wa Mwanafunzi Wanaoweza Kumtembelea Mwanafunzi Shuleni Pamoja na namba zao za simu.


**NB*: Shule haitoi chakula maalum (Special Diet); Hivyo chakula kitakachopikwa jikoni, ndicho kitakacholiwa na wanafunzi wote.Hairuhusiwi kula chakula nje ya shule; hii ni kwa usalama wa afya ya mwanafunzi.***

***Soma kwa makini maelekezo/ maagizo haya na uyatekeleze kikamilifu.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**



**STEPHEN J. MZIMYA**
**MKUU WA SHULE**
**0755 428 626 / 0735 428 626 / 0782 728 427**



**HABARI ZA MWANAFUNZI**
1. JINA LA MWANAFUNZI …………………………………………………………………
2. KABILA …….……………………………
3. TAREHE YA KUZALIWA…………… MWEZI …………. MWAKA ……………………
4. AMEZALIWA KATIKA WILAYA YA …………………………MKOA WA ………………
5. DINI ……………………. ………………………………………………………..
6. JINA LA MZAZI/MLEZI ….……………………………………………………………
7. ANWANI YA MZAZI/MLEZI: S.L.P ……………………. KIJIJI………………….
KATA ……………………. …. WILAYA………………………….
Namba ya/za Simu ………………………………………………………………………
8. KAZI YA MZAZI/MLEZI ………………………………………………………………
**Afya ya Mwanafunzi** (Kama ana ugonjwa unaohitaji uangalizi uandikwe. Taja udhaifu wowote wa mwili au afya yake na uambatanishe cheti cha daktari )
…………………………………………………………………………………………………

**AHADI YA MWANAFUNZI NA MZAZI KUHUSU SHERIA ZA SHULE YA SEKONDARI NANGA.**
**Mimi …**……………………………………………..……………
Kidato cha **V** Tahasusi **(CBG/HGK/HKL/HGE/HKL)** Mwaka…………………………………..
Nimezisoma na kuzielewa sheria na kanuni zilizoainishwa katika fomu yenu maalum. Ninakiri kuzipokea na kwamba nitazitekeleza.Endapo nitaenda kinyume na sheria na kanuni hizi, Uongozi wa Shule unichukulie hatua za kinidhamu kulingana na maelekezo ya kwenye Fomu elekezi niliyopewa.
**SAHIHI YA MWANAFUNZI ……………………….. TAREHE …………………………**

**UTHIBITISHO WA MZAZI/MLEZI**
Mzazi/Mlezi ……………………………………………………………………………
Ninathibitisha kuipata fomu ya Sheria za Shule yenu nimezisoma na kuzielewa kwa kina.
Ninaahidi kushirikiana na Shule katika kumlea mwanangu huyu katika misingi ya sheria hizo:
**SAHIHI YA MZAZI/MLEZI: ……………………………….TAREHE ……………………**

**Sehemu za Picha za Wazazi/Walezi**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Picha | | | |
| Jina | | | |
| Simu | | | |

**THE MEDICAL EXAMINATION FORM SHOULD BE COMPLETED BY GOVERNMENT MEDICAL OFFICER**

FROM THE HEADMASTER/HEADMISTRESS
NANGA SECONDARY SCHOOL,
P.O BOX 108,
IGUNGA.
Mobile No. +255 (0) 755 428 626 / +255 (0) 782 728 427
TO THE MEDICAL OFFICER,
RE: MR/ MISS/MIS
………………………………………………………………………………………..

**MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a government medical officer).

Please examine the above-named person as to his/her Physical and Mental fitness for full time learning.

a) Eye Sight ……………………………………………………………………………
b) Hearing …………………………………………………………………………
c) Limb ………………………………………………………………………………
d) Speech ……………………………………………………………………………
e) Venereal Diseases ………………………………………………………………
f)Leprosy……………………………………………………………………………
g) Epilepsy …………………………………………………………………………
h) Blood Test ………………………………………………………………………
i) Stool Examination ………………………………………………………………
j) T.S Test……………………………………………………………………………
k) Asthma…………………………………………………………….............……
l) Anaemia…………………………………………………………….............……
m) Chest ……………………………………………………………………….....
n) Operations ………………………………………………………………………
o) Serious Accidents ………………………………………………………………
p) Any Other Infection
Neuroses …………………………………………………………………………
Other Serious Diseases ………………………………………………………………….
Pregnancy …………………………………………………………………………

The diagnosis reveals that the above-named person is physically and mentally fit/ unfit for full time studying

Name and signature of the medical Officer.

________________________________________________________date______